



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGATANZANIA



**TANGAZO MAALUMU**

**MAOMBI YA MTIHANI WA USAJILI NA LESENI AGOSTI, 2024**

***Dodoma; 21 Mei 2024***

Ofisi ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania, inawatangazia wahitimu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa Usajili na Leseni kuwa, dirisha la maombi ya Mtihani litafunguliwa rasmi kuanzia tarehe **01/07/2024** hadi tarehe **14/08/2024**.

Maombi yatafanyika kupitia mtandao kwa kutumia mfumo wa Baraza (<https://tnmcis.tnmc.go.tz>) Kila mwombaji atatakiwa kujisajili na kulipia kiasi cha Shilingi **150,000/=** kwa wale wanaoomba kufanya mtihani huu kwa mara ya kwanza na Shilingi **75,000/=** kwa wanaorudia.

**Waombaji wote mnajulishwa kuzingatia masharti yafuatayo;**

- Muombaji anatakiwa kuhakikisha amekamilisha usajili wa awali (***Indexing***) kwa mujibu wa kifungu cha **14 (1)** cha kanuni za mafunzo.
- Kuzingatia uwekaji wa mahitaji yote ya maombi ambayo ni ***Passport Size (45x35mm Blue Background)***, Majina sahihi yanayoendana na cheti cha kuhitimu elimu ya Sekondari pamoja na namba ya **NIDA**
- Mtihani utafanyika katika vituo vitakavyopangwa katika mikoa ya **Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya na Dodoma.**

*Imetolewa na*

**Ndimmyake Mwakapiso**  
**Ofisa Uhusiano na Mawasiliano TNMC**